

## CHUO CHA SERIKALI ZA MITAA



### MWALIKO WA ZABUNI KWA AJILI YA KUPATA FUNDI SANIFU WA KAZI YA UJENZI WA DARASA LA WANAFUNZI MIA TANO AROBAINI, UKARABATI WA MAJENGO MBALIMBALI YA CHUO NA UKARABATI WA MFUMO WA MAJI SAFI NA MAJI TAKA KATIKA CHUO CHA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

Tarehe: 16 Agosti, 2021

1. Mwaliko huu wa Zabuni unafuata Tangazo la Jumla la Ununuzi (TJU) kwa ajili ya Chuo cha Serikali Za Mitaa kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021 uliotangazwa katika mfumo wa ununuzi wa kielektroniki (TANePS) na kuridhiwa na Mamlaka ya Ununuzi wa Umma (PPRA) tarehe 13<sup>rd</sup> October, 2020.
2. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetenga fedha kwa ajili ya uendeshaji wa Chuo cha Serikali za Mitaa katika mwaka wa fedha 2020/2021. Inakusudiwa kuwa sehemu ya fedha hizo zitatumika kugharamia malipo halali chini ya mkataba ambao utatolewa katika mwaliko wa Zabuni hii.
3. Hivyo, Chuo cha Serikali za Mitaa kinakaribisha maombi kutoka kwa mafundi sanifu wa ujenzi kwa ajili ya kufanya kazi ya Ujenzi na ukarabati kama zilivyo ainishwa kwenye kichwa cha habari hapo juu kwa kutumia utaratibu wa "Force Account". Fundi sanifu anatakiwa kushiriki katika Zabuni ya kufanya kazi hii kwa kutumia mtandao wa ununuzi wa kielektroniki (TANePS).
4. Unakaribishwa kuleta Zabuni yako iliyojazwa bei kwa ajili ya utekelezaji wa kazi kama ilivyoielezwa katika Mchanganuo wa Makadirio ya Kazi (MMK) na kufafanuliwa ipasavyo katika sehemu ya II ya Kitabu cha Zabuni. Gharama ya kazi haitahusisha ununuzi wa vifaa vyovyote vya ujenzi (mahunzi) hivyo, oneshwa mchanganuo wa gharama ya ufundi tu kwa kazi zote kwa kuzingatia maelekezo ya mahitaji yaliyoambatanishwa pamoja na zabuni hii. Mchanganuo wa kazi katika mwaliko wa Zabuni umeainishwa kwa kina katika **Zabuni Na. PA/080/2020/2021/W/01 Lot 01-07.**

5. Fundi sanifu anatakiwa kushiriki katika Zabuni ya kufanya kazi hii kwa kutumia mtandao wa ununuzi wa kielektroniki (TANePS) ikiwa ni takwa la sheria ya Ununuzi, hivyo vitabu vya Zabuni havitauzwa na vitakuwa kwenye mfumo wa TANePS.
  
6. Unaombwa kushiriki katika Zabuni tajwa hapo juu na siku ya mwisho ya kuwasilisha Zabuni kupitia mfumo wa ununuzi wa kielektroniki (TANePS) ni siku ya Jumatatu ya tarehe 23 Agosti, 2021 kabla ya saa saba na nusu (7:30) mchana. Zabuni zitafunguliwa kwa njia za kielektroniki kwa kutumia mfumo wa ununuzi wa kielektroniki (TANePS) na washiriki wa Zabuni watapata fursa ya kuona taarifa ya ufunguzi kwa njia ya mfumo wa TANePS.

  
Dkt. Mpamila M. Madale

**MKUU WA CHUO**

Mkuu wa Chuo  
Chuo cha Serikali za Mitaa-Hombolo  
S. L. P. 1125,  
DODOMA